


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu

*Dkt. Lina Akaka, PhD[1*] & Dkt. Sheila Wandera- Simwa, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Catholic University of Eastern Africa, S. L. P. 62157-00200. Nairobi, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100 – 20300. Nyahururu, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-4376-5794; Barua pepe ya mawasiliano: akakalina2016@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*26 Agosti 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Bembelezi, Walengwa, Washiriki, Ujumbe, Watikuu.*

**IKISIRI**

Nyimbo zikiwa za watoto, inatarajiwa kuwa walengwa watakuwa watoto wenyewe kwa kuwa maudhui yaliyomo yatawalenga. Bembelezi zilizotafitiwa katika tamaduni mbalimbali ulimwenguni zinaonyesha kuwa ujumbe uliyomo huwalenga watoto na wakati mwingine, mama na baba zao. Kimsingi, wanawake, kando na kuzitumia katika shughuli za kubembeleza watoto, huzitumia pia kama jukwaa la kujieleza na kutakasa mioyo yao kutokana na uchungu, mtamauko na mfadhaiko wa mawazo uliosababishwa na matatizo ya kindoa kutokana na mifumo ya kibabedume inayoendelezwa katika baadhi ya jamii. Makala hii inachunguza diskosi zinazojitokeza katika bembelezi za Watikuu ili kubaini walengwa wa ujumbe uliomo. Lugha inayotumiwa na wanawake katika uimbaji wa bembelezi hizi inatilia shaka iwapo ujumbe uliomo unalenga tu watoto au mna watu wengine wanaolengwa kando na watoto.

**APA CITATION**

Akaka, L., & Simwa, S. W. (2022). Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 288-296. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817.

**CHICAGO CITATION**

Akaka, Lina and Sheila Wandera- Simwa. 2022. "Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 288-296. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817.

**HARVARD CITATION**

Akaka, L., & Simwa, S. W. (2022) "Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 288-296. doi: 10.37284/jammk.5.1.817.

**IEEE CITATION**

L. Akaka, & S. W. Simwa, "Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 288-296, Aug. 2022.

**MLA CITATION**

Akaka, Lina & Sheila Wandera- Simwa. "Walengwa wa Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Aug. 2022, pp. 288-296, doi:10.37284/jammk.5.1.817.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

## UTANGULIZI

Bembelezi ni kifaa muhimu cha mawasiliano kati ya mama na mtoto na huboresha mtagusano wao na kumfundisha mtoto lugha ya mama. Bembelezi ni hazina ya misimbo ya kitamaduni ambayo ina mkusanyiko wa ujumbe wa kitamaduni na kijamii ambao hukubalika katika jamii husika. Elimu ya kitamaduni huanza na misimbo hii ya kitamaduni kupitia kwa bembelezi (Kaya na Özkut, 2016). Mawazo ya Kaya na Ozkut yanadhihirisha kuwa bembelezi hubeba ujumbe ingawa walengwa wa ujumbe hutofautiana kutoka jamii hadi nyingine huku mtoto akiwa mlengwa mkuu. Bembelezi za Watikuu zinaonyesha ujumbe uliomo hulenga watu mbalimbali katika jamii wakiwemo mavyaa, wifi, nyanya ya mtoto, baba yake, mama yake, jirani, msichana aliyeposwa, rafiki ya mwimbaji na wengineo. Bembelezi hizo hulenga watu wengi zaidi katika jamii hiyo kuliko bembelezi za jamii nyingine ambazo hulenga watu wachache. Akyol (2014), anahoji bembelezi hufaraguliwa kwa urahisi kuliko nyimbo nyingine za kitamaduni. Sifa hii ndiyo inayozifanya ziwe kifaa muhimu mikononi mwa wanawake kwani huzitumia kueleza mtamauko wao, mawazo, mshinikizo wa kijamii na utata unaosababishwa na pingamizi za ndani kwa ndani. Kila mama huwa msanii na kila bembelezi inafaa kuchukuliwa kama kazi asilia ya kisanii, anasema Akyol (2014). Makala hii inabaini walengwa wa ujumbe katika bembelezi zinazoimbwa na wanawake Watikuu, wenyeji wa Kisiwa cha Faza kilicho ndani ya Kisiwa cha Pate, Mashariki mwa Kisiwa cha Amu. Matokeo ya tafiti zilizotangulia kuhusu bembelezi yanaonyesha kuwa ujumbe katika bembelezi huwalenga watoto; makala haya yanalenga kubaini walengwa wengine kando na watoto hususan ikikumbukwa kwamba lugha inayotumiwa ni tata na kutilia shaka iwapo kweli ujumbe mzito uliyomo unaweza kuwa unalenga mtoto peke yake.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti uliongozwa na nadharia ya ethinografia ya mawasiliano kama ilivyoelezwa na Saville-Troike (2003) na mhimili wa 'washiriki' ukatumiwa kubaini walengwa katika bembelezi za Watikuu. Kipengele cha washiriki ni cha msingi sana katika tukio lolote la mawasiliano. Kwa mujibu wa Saville-Troike, katika tukio lolote la mawasiliano, ni muhimu kufahamu wanaoshiriki tukio hilo. Anaendelea kueleza kuwa kategoria hii inajumlisha sio tu wazungumzaji bali pia wasikilizaji na wasiokusudiwa kusikiliza. Bembelezi ni tukio la kimawasiliano ambalo kwa hali ya kawaida hukusudiwa watoto. Hata hivyo, baadhi ya bembelezi ulimwenguni zinaonyesha kinyume; nyimbo hizi huwa na hadhira tuli, iliyokusudiwa kupokea ujumbe na isiyokusudiwa. Hadhira zote mbili huchukuliwa kama washiriki katika tukio hilo la mawasiliano na kwa kuwa walezi huziimba kwa sauti wanapobembeleza watoto, basi ujumbe hufikia hadhira zote mbili. Watafiti walibaini washiriki wote wa kila tukio la bembelezi; waliokusudiwa ujumbe na wasiokusudiwa.

## MBINU ZA UTAFITI

Watafiti walitumia mbinu za uteuzi wa kimaksudi na kuelekezwa kuteua sampuli ya wanawake 12 waliowaimbia bembelezi katika vikundi lengwa viwili vya mjadala. Kati ya bembelezi 20 walizoimba, bembelezi nane ziliteuliwa kwa mbinu ya kujichagulia kwa hiari ili kutafitiwa. Bembelezi zilizotafitiwa ziliteuliwa kwa misingi ya walengwa waliokusudiwa kupokea ujumbe.

## MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa bembelezi za Watikuu zina walengwa mbalimbali katika jamii kando na watoto. Wanawake katika jamii hii huzitumia kama jukwaa la kuwasuta watu waliowakosea, kuwausia watoto wao, kueleza hisia na mitamauko yao. Bembelezi zimekuwa jukwaa la kusuluhisha mizozo baina ya wanawake katika jamii ya Watikuu. Wanawake huzitumia pia kulalamika kuhusu dhuluma walizofanyiwa na mtu fulani na kupitisha ujumbe kwa watu tofauti. Bembelezi hutumiwa kuwausia watoto, mabinti, kurekebisha tabia, kueleza kuhusu matatizo ya kindoa na kutakasa hisia mlezi anapokuwa na uchungu wa moyo. Chiraghdin (1973) katika Abdalla (2012) anasema, "Na mtu akiwa na dhiki ya moyo, hapana njia bora kuliko kulitoa alilonalo moyoni. Na kwa Mswahili, njia nzuri zaidi ni ya kutongoa kwa mashairi na nyimbo, akiwa ajua."

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**Rafiki kama Mlengwa**

Kimsingi, bembelezi za tamaduni nyingi ulimwenguni huimbiwa watoto na ujumbe uliomo hulenga watoto. Hata hivyo bembelezi za Watikuu hulenga watu tofauti tofauti katika jamii kando na watoto. Bembelezi ifuatayo ina washiriki wanne, watu watatu ambao ujumbe ulilenga na mwimbaji bembelezi yenyewe. Mawasiliano ni tukio kwa mujibu wa Saville-Troike (2003) na anahoji ni tukio ambamo mtumaji na mpokeaji ujumbe hushiriki. Katika muktadha wa tukio la mawasiliano la uimbaji wa bembelezi, washiriki wote hubadilikabadilika. Hii ina maana kwamba nafasi ya mwimbaji inaweza kukaliwa na mlezi yeyote wa kike kama vile mama ya mtoto, wifi, dada mkubwa, nyanya hali kadhalika shangazi.

Mshiriki mkuu wa nafasi ya mlengwa ni mtoto. Kila bembelezi humlenga kwa sababu mtoto huimbiwa kwa kusudi la kumbembeleza. Hata hivyo baadhi ya bembelezi hubeba ujumbe unaowalenga watu wengine katika jamii na mtoto akafaidi tu kutokana na melodia. Katika bembelezi ifuatayo iliyo na beti tatu, watu watatu wanalengwa; rafiki ya mama yake mtoto, kaka ya mtoto anayeimbiwa na mtoto mwenyewe. Katika ubeti wa kwanza, ujumbe uliomo unamlenga rafiki ya mwimbaji. Mama ya mtoto anamlaumu rafiki kwa kuwa gawadi wa bintiye na kumpa mwanamume ambaye aliuharibu ubikira wake. Anajuta kwa kumtendea mema kama rafiki kumbe anamla ndani kwa ndani na sasa amesababisha kuharibika kwa binti yake.

*Howa Nchocho Howa x2*

*Nilikufanya rafiki kakupa siri za ndani*

*Kisha kakufanya wanda kakutia matoni*

*Karama uwe ni simba hunila ndani kwa ndani*

**Mtoto na Kaka yake kama Walengwa**

Katika ubeti wa pili ufuatao, mwimbaji anaendeleza ujumbe wa ubeti wa kwanza katika mshororo wa kwanza ubeti ufuatao. Anauliza karatasi iliyolowa maji, atakayeisoma ni nani? Hili ni fumbo linalomlenga bintiye, kuwa atakayemwoa ni nani baada ya kuharibiwa ubikra? Ujumbe katika mishororo miwili ya mwisho unamlenga mtoto wake wa kiume Asumani ambaye mke wake humtusi mama huyu pamoja na jamaa zake waliofariki. Mama anazungumza na mtoto anayebembeleza (Rukiya) katika ubeti wa mwisho. Anamhimiza mtoto kukua ili amfunze mambo ya utu uzima asije pia akaharibiwa ubikira angali mdogo kama dada yake.

*Karatasi ya maini mwenye kusoma ni nyani?*

*Alonitakia imi ni mwanangu Asumani*

*Kuchukua va ahera kuvaeta duniani*

*Kua mwanangu Rukiya nikusomeshe skuli*

*Nikufundishe ubembe uhadaliye vavuli*

*Ni nyani afungudhieyeo nami nichie kufuli*

**Mavyaa na Mtoto kama Walengwa**

Washiriki katika bembelezi ifuatayo ni watatu; mwimbaji mwenyewe kama mshiriki, mavyaa wa mwimbaji na mtoto wake Ahamad. Ujumbe katika ubeti ufuatao wa bembelezi ya pili unamlenga mavyaa wake. Mwimbaji amembandika mavyaa yake jina Tima Tumu kama mbinu ya kufumba ujumbe anaopitisha usiwe wa moja kwa moja. Tima Tumu alikuwa akimtukana mkazamwana wake pamoja na watu wa kwao wote. Katika matusi hayo, hakuwasaza wazee kwa watoto, wote walitukanwa, isitoshe alikuwa akimsengenya na watu.

*Howa nchoncho howa x2*

*Yana Tima Tumu alinichukana*

*Hakuchusaza vazee kwa vana*

*Asojua ruli simpe maana*

Katika beti mbili za mwisho zifuatazo, mwimbaji anamwambia mtoto wake Ahamad kwamba asije akawa kama nyanya yake akaanza kusema mambo machafu. Alimweleza mtoto mengi kuhusu nyanya yake, kisha akamwambia kwamba iwapo hasadiki mambo aliyomwambia awaulize wambeya halafu asikilize vizuri kila lisemwalo. Utamaduni wa wanawake kutumia nyimbo kama jukwaa la kujieleza unadhihirika pia katika bembelezi za

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

Watikuu. Isitoshe, utamaduni huo unadhihirika katika bembelezi za jamii nyingine kote ulimwenguni. Huenda ni kwa sababu ya historia ndefu ya wanawake kukandamizwa. Senkoro (2005), anakubaliana na mawazo hayo anapohoji kuwa bembelezi zilitumiwa na wanawake kueleza hisia zao kuhusu maisha yao ya ndoa.

*Ahamad usinene maneno machafu*

*Kama huyasadiki kavulize vatu*

*Usiveke nyama katika siafu*

*Mwana Ahamad sikiza lambwao*

*Usikize ngoma sura ziliavo*

*Mahaba matamu ataka pumbao*

**Wifi kama Walengwa**

Kuna jumla ya washiriki watatu katika bembelezi ya tatu; mwimbaji, mtoto na wifi za mwimbaji. Mtoto ndiye anayeimbiwa bembelezi, ingawa ujumbe haumlengi, anafaidi kwa melodia tu. Trehub na Prince (2002) wanasema melodia za bembelezi ndizo hubembeleza na kuleta hisia za utulivu kwa mtoto na kumsababisha kulala. Ujumbe katika bembelezi hiyo unawalenga dada za mume wa mwimbaji, walikuwa wakiendeleza umbeya kumhusu kijijini. Wifi za mwimbaji walikuwa wanamsengenya na kumsingizia maneno mengi. Mwimbaji anasema anajua mambo ambayo wanasema na anawahimiza waendelee hadi maneno yawakauke.

*Howa nchocho, howa x2*

*Kuna chungu kiandisiwa huchokocha siku zote*

*Mwishiza mai jabia na kuni makoko yote*

*Mja hupanga kupata huva hataki akose*

*Muifanyiza wajuzi hapo siasa hamuziisi*

*Chungu mukiandisecho hulalamika vapishi*

*Mutazidi kutotea ama mutaveka iti*

Uhasama wa akina wifi dhidi ya mke aliyeolewa ni jambo la kawaida katika jamii ya Watikuu kama walivyosema wasailiwa. Dada za mume wakiwa hawakuolewa au kutalikiana na waume zao huwa wanatatiza ndoa za kaka zao wakiwa pale nyumbani. Hali hii hutokea kwa sababu ya kumwonea mke wa kaka yao wivu kufuatia vile anavyotunzwa na kaka yao. Kwa mujibu wa wasailiwa, wakati mwingine tofauti hizo hutokana na hali kwamba kaka hukosa uwezo wa kuwakimu kwa hivyo dada zake humwona mke wake kama kizingiti kinachowazuia kunufaika kutokana na mali yake.

Hali kama hii na nyinginezo katika ndoa huwafanya akina mama kueleza na kutakasa hisia zao kwa bembelezi. Hassan (2010) anadhihirisha hilo anaposema kwamba akina mama wa Kiiraq hutumia bembelezi kutoa hisia zao kuhusu hali ya vita. Hueleza kwa bembelezi vile vita vinavyo watenganisha na waume zao na kuwafanya wapitie hali ngumu bila wao. Wanawake hawa pia huomboleza kuhusu watoto wao wakubwa wa kiume ambao huwa wameungana na baba zao katika vita kwa lengo la kutetea nchi yao.

**Binti Aliyeposwa kama Mlengwa**

Washiriki katika bembelezi ya nne ni watatu. Mama ndiye mwimbaji, mlengwa wa ujumbe ni binti aliyeposwa na mtoto, ambaye anafaidi tu kwa melodia. Katika bembelezi, mama alikuwa anamshauri binti yake kuhusu umuhimu wa mume. Mama alimbembeleza mtoto ambaye alikuwa analia na wakati huohuo kutoa ushauri kwa binti yake. Mama anamweleza bintiye kuwa mwanamume ni mtu muhimu kwa mwanamke anapokuwa naye, humsitiri kwa shida na kwa raha. Katika beti zifuatazo, mama anamuusia binti yake asikate tamaa anapopitia katika changamoto za ndoa, kwani lolote alilompangia Mungu hufanyika.

*Howa nchoncho howa x2*

*Bamba ni kitu muhimu kwa kusi na kaskazi*

*Na nyumba pia hudumu hupungua nyingi kazi*

*Waume hujifahamu mambo yote ni wazazi*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

*Howa nchocho howa x2*

*Bamba ndilo la kufaa kwa mvua na hata jua*

*Nyumba ni yako haswa kwa mtu atakutowa*

Kwa mujibu wa wasailiwa, Waswahili wana desturi ya kuusia mabinti kuhusu unyumba, ndoa na usafi. Hufanya hivyo unyagoni ambapo huwa wanaimba nyimbo kama vile chendanaye, lelemama na vugo za kutilia mkazo mafundisho. Bembelezi hutumiwa pia kama jukwaa la kuwapa mabinti wosia kando na kubembeleza watoto katika jamii ya Watikuu. Bembelezi za jamii nyingine ulimwenguni zinaonyesha kwamba akina mama walitumia bembelezi kuwausia watoto waliokuwa wakibembelezwa kama vile Mackinlay na Baker (2005) wanavyosema kwamba watoto waliusiwa kuwa waadilifu na kuelezwa kuhusu ulimwengu watakaokabiliana nao huku mama akitaka mtoto kuwa na nidhamu ili apate kufaulu maishani.

**Mtoto kama Mlengwa**

Bembelezi ya tano ina washiriki wawili, mama na mtoto. Mlengwa ni mtoto aliyeimbiwa bembelezi na mama. Ujumbe unamlenga mtoto hata ingawa haelewi mambo anayoambiwa, hata hivyo hulala kwa sababu ya sauti nyororo ambayo mama hutumia anapoimba. Loewy na wenzake (2013) wanahoji mtoto huendelea kufarijiwa na kutulizwa na sauti ya mama miezi mingi baada ya kuzaliwa; na hiyo ndiyo sababu bembelezi huwatuliza hata ingawa hawayaelewi maneno. Katika ubeti wa kwanza wa bembelezi ifuatayo, mama anamnyamazisha mtoto kwa kumwambia kwamba asilie kwa kuwa ni usiku na mashetani huzunguka, asitoe sauti wakaichukua.

*Howa nchocho howa x2*

*Silie usiku ndia zina vachu*

*Zina vaswalina na vachavo Mungu*

*Mame mwanangu niombea Mungu siku ya utungu*

Katika ubeti wa pili ufuatao mwimbaji anamwambia mtoto vile ametaabika akimlea; mitulinga imemtoka. Mama alimwambia mtoto hali yake ya kiuchumi ni ya chini na hana urithi wa kumpa. Mara nyingi akina mama waliwaeleza watoto dhiki zao katika bembelezi kama njia ya kutakasa hisia.

*Howa nchoncho, howa x2*

*Silie mwana kilio cha daima*

*Hunitoa mchilinga nami michilinga sina*

*Sina urithi mwanangu na imi mwana bibie mbwainya*

Katika ubeti wa mwisho ufuatao, mama anamweleza mtoto kwamba akikua na kuanza kwenda shambani, awe akibeba chombo cha maji na unga wake mkobani. Anamuusia kuwa asiwe akitia mapenzi moyoni kwani yanaweza kumwua.

*Howa nchoncho, howa x2*

*Ukenda hondeni tukuwa bori na daba*

*Na vunga vako taani japokuwa ni kibaba*

*Usiatie ruhuni yatakuvua mahaba*

**Mume kama Mlengwa**

Bembelezi ya sita ina washiriki watatu: mtoto, baba na mama ambaye ndiye mwimbaji. Mtoto anafaidi kwa melodia huku ujumbe ukimlenga mume. Mtoto ndiye anaimbiwa bembelezi hii, ingawa ujumbe uliomo haumlengi, anafaidi kutokana na melodia yake. Gunes na Gunes (2012) wanasema mtoto huwa haelewi maneno yanayosemwa katika bembelezi lakini hufaidi kwa vipengele vya kimuziki kama vile kiimbo, toni na kupanda na kushuka kwa sauti ambavyo huchochea usingizi. Ujumbe katika bembelezi hii unamlenga mume ambaye alikuwa amemwacha mke wake na kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Katika bembelezi hiyo ifuatayo, mama anambeza mume wake kwa kusema:

*Howa nchoncho howa x2*

*Huliya mwana huliya*

*Husaliwa na mayuto*

*Ungaufuta ushingo*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

*Howa nchoncho howa x2*

*Unacho chembe unacho*

*Alhamdulilahi kwa Mola nishukurie*

*Leo hupemba mwanangu*

*Nduza vanisaidie*

Kwa mujibu wa wasailiwa, urafiki wa mume huyo na mwanamke wa kando haukudumu. Mambo yaliharibika na akataka kurudi kwa mke wake lakini mke akawa hamtaki tena. Mwimbaji anambeza mume wake na akimweleza kuwa aliendelea kueleza kuwa anajuta na uchungu anao moyoni kwa kukosa yote. Bembelezi hii inaakisi uchungu wa mama kwa sababu ya kitendo ambacho mume wake alifanya. Anatumia bembelezi kutakasa hisia zake na kueleza yaliyomkaa moyoni. Mackinlay na Baker (2005) wanasema akina mama wengi hupitia katika mifadhaiko, hofu na masikitiko ya mara kwa mara ambayo yanaweza kupunguzwa kupitia kwa uimbaji wa bembelezi.

**Waume, Jirani na Mtoto kama Walengwa**

Washiriki watano wamejitokeza katika bembelezi ya saba. Washiriki hao ni mtoto, Mahadhi, Simai, Nyazira na mwimbaji. Kama ilivyo katika bembelezi nyingine za Watikuu, mtoto anafaidi tu kutokana na melodia peke yake katika bembelezi hii huku ujumbe ukiwalenga washiriki wengine. Mwimbaji ambaye ni Mwanahalima aliolewa ndoa ya kwanza kwa mume wake Simai lakini akaachana naye na kuolewa na mume wa pili kwa jina Mahadhi. Nyazira alikuwa jirani wao. Katika ubeti ufuatao, ujumbe katika bembelezi unamlenga Simai aliyekuwa mume wa kwanza wa Mwanahalima, mwimbaji wa bembelezi.

*Howa nchoncho howa x2*

*Simai ishe wanangu ukipita nivilia*

*Na kama sikukutika ni yiva sikukusikia*

*Nyuka utoke Mahadhi boke ‘mekuzungukia*

Mume wa kwanza wa Mwanahalima aliitwa Simai na mume wa pili aliitwa Mahadhi. Mwanahalima anamwambia Simai aliyekuwa mume wake pia baba ya watoto wake kwamba, akipita kisha amsalimie na akose kujibu salamu zake, ajue kuwa hakumsikia. Mume wa pili Mahadhi anaamrishwa kuondoka kwa kuwa mume wa kwanza ambaye anamwita boke kimafumbo amekuja, hivyo ampe nafasi pia. Kwa mujibu wa wasailiwa, boke ni aina ya ndege ambaye makinda wake wakikaribiwa, huwakinga kwa kumpiga adui kwa mabawa yake. Mwanamke huyo anamlinganisha mumewe wa kwanza Simai na boke, kwamba sasa anataka kumrudia mkewe na hatakuwa na budi kumkinga kutokana na yeyote aliyemchukua.

Kulingana na wasailiwa Simai kutaka kurudi kwa mke wake hata baada yake kuolewa na mume mwingine si jambo geni katika utamaduni wa Watikuu. Wanaume huwa huru kumregesha mke aliyeachana naye iwapo ndoa aliyo nayo haikumwendea vizuri na akarudi kwao au kukosa ndoa baada ya kuachana kwao. Hali hii inatokea pia katika bembelezi ya sita ambapo mume alitaka kumrudia mke wake tena baada ya kumwacha lakini mke akamkataa. Katika ubeti ufuatao, Mwanahalima anasema yeye ni kama bahari, amekosa kutulia. Kulingana na wasailiwa, neno bahari limetumiwa kimafumbo kwa maana ya mke wa kila mtu, yaani yeye yuko wazi kwa kila mwanamume, hawezi kueleweka. Mwanahalima ni kama bahari ipitwayo na kila chombo cha bahari; mashua, jahazi, kidau, boti, merikebu hali kadhalika meli. Katika mshororo wa pili anaeleza nyumba yake huwa kama jela ambayo ina milango sita, mwanamume akishaingia pale humfungia akammalizia haja yake na kuondoka. Kwa kuwa nyumba yenyewe ina milango sita, mwanamume mmoja akiingia kwa kutumia mlango mmoja aliyekuwa ndani anatokea kwa mlango mwingine. Katika mshororo wa mwisho, anaeleza kuwa Simai, yule mume wake wa kwanza akiwa amelala ndani mwanamume yeyote aliye na haja huwa anaingia ndani naye akammalizia haja yake.

*Mwanahalima bahari mekosa kutanganyika*

*Nyumba hujenga jela na milango yake sita*

*Simai huvauyele na atakao akapita*

Katika ubeti wa mwisho ufuatao, Mwanahalima ana ujumbe kwa mke wa mmojawapo wa wateja wake. Anasema:

*Siniate imi pweke nawe Nyazira nena Usiniache*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

*Kwa viumbe ni maovu Kirama huandika mema*

*Hulitumbuiza jembe mwakani silimi tena*

Nyazira ni jirani ya Mwanahalima. Mwanahalima anamwambia asimuache peke yake, amtetee, iwapo atalaumiwa. Anatambua kuwa yote ambayo anafanya ni maovu machoni mwa binadamu lakini anasema kwamba Mungu humwandikia mema kwa sababu anafanya anayofanya kwa nia ya kujitafutia riziki. Mshororo wa mwisho, *hulitumbuiza yembe mwakani silimi tena* ni fumbo, kulingana na wasailiwa lina maana kwamba anauuza mwili wake zaidi ili asifanye mambo hayo tena mwaka utakaofuatia.

**Mume, Mkemwenza na Mtoto kama Walengwa**

Washiriki katika bembelezi ya nane ni wanne na walengwa ni watatu wakiwemo mume, mkemwenza na mtoto. Mwimbaji ni mshiriki anayetekeleza tukio la uimbaji. Katika ubeti wa kwanza ufuatao, ujumbe unamlenga mtoto. Mama anamwambia binti yake kuwa alimlea kwa shida, akinywa maji kwa unga mchache hadi akawa mwanamke wa kulinganishwa na irumani; ng'ombe wa maziwa, wa kuleta faida. Kulingana na wasailiwa, irumani ni ng'ombe anayekamuliwa maziwa. Mama anamlinganisha bintiye na ng'ombe kama huyo, yaani awe mwanamke wa faida wakati wote, mwenye thamani na kutoa yaliyo mazuri peke yake vile alivyomfundisha. Katika mshororo wa mwisho, anasema ng'ombe ni wa mchungaji, yaani mtoto ni wa mtu anayemlea, yeye ndiye humjenga mtoto akainukia kuwa mwadilifu kama vile mchungaji anavyochunga mifugo wake na kuwafunza nidhamu malishoni. huku mwimbaji ambaye ni mama ya mtoto anamkumbusha mtoto taabu alizopitia akimlea na kumhimiza akue awe mtu wa faida kama ng'ombe wa maziwa.

*Howa nchoncho howa x2*

*Si bure mambo, mwanafunzi naliyekufunda*

*Kwa bori a mai na taa ya vunga iva irumani*

*Ng'ombe wantunga*

Ubeti wa pili ufuatao umebeba ujumbe kwa mume wa mwimbaji. Mwimbaji alimbeza mume wake akisema samaki na kamba wote ni watamu. Kamba ni aina ya samaki kwa mujibu wa wasailiwa. Hao samaki wawili wakiliwa ndipo mtu hugundua kila mmoja ana ladha tofauti, kwa kuwa utajiramba vidole hata pasiwe na mabaki. Mama huyu anajaribu kumwambia mume wake kuwa kila mwanamke ni mzuri kwa namna moja au nyingine na itakuwa bora aridhike na yule wake kwa kuwa kila mmoja huwa na ladha yake nzuri tofauti na ya mwingine, asifanye tamaa. Mama anasikitika kwamba yule mume wake alipoondoka, ilikuwa ni kama kukatiwa mti kama inavyodhihirika katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa pili ufuatao. Komba ni mnyama anayeishi mitini, mti ukikatwa, komba hukosa makao. Basi yule mama ni kama huyo komba kwa sababu mume aliyekuwa anamsitiri amechukuliwa na mwanamke mwingine; sasa ni kama amekosa makazi. Wazo hili linajitokeza katika bembelezi ya nne mume anapolinganishwa na bamba au paa; wazo hili linafafanua zaidi mtazamo wa wanawake Watikuu kuhusu waume na ndoa. Wanaume ndio nguzo ya mwanamke, sitara na hifadhi yake; hivyo mwanamke akikosa mume huonekana kukosa cha kumstiri.

*Howa nchoncho howa*

*Si bure mambo, samaki na kamba tamu*

*Tafauti ukila huramba, husavi kafiti*

*Masikini komba ukachiwa nti*

Katika ubeti wa tatu ufuatao, mwimbaji anaomboleza kwamba licha ya kumtunza mumewe, alitokea hasidi akampokonya huyo mume. Gunes na Gunes (2012) wanasema katika hali kama hiyo, mama hubuni maudhui ya bembelezi kutokana na tajriba anazopitia maishani; mara kwa mara maudhui katika bembelezi zake humrejelea mumewe, mavyaa wake, mikasa ya kiasili, vita, dhiki na furaha zake. Mwimbaji anatumia fumbo la mmea wa mbatata kueleza kisa chake, mmea huo ukiwa fumbo linalomaanisha mumewe. Katika ubeti ufuatao, mwimbaji anaeleza alitokea hasidi akaukanyaga mbatata wake.

*Nami nali nao wangu mbatata eeh*

*Katoka hasidi akaulizata*

*Naliliya yangu bahati kupata*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

Ubeti wa nne ufuatao ujumbe katika ubeti wa tatu. Mwimbaji anaendeleza kilio dhidi ya mume wake huku akimlenga mkemwenza wake ifuatavyo:

*Si bure mambo, nali nao wangu mkorosho*

*Katoka hasidi kaupiga moto*

*Naliliya yangu bahati ni chocho*

*Si bure mambo, usiku wa jana*

*Nilihangaika kaandika chai ndani ya*

*Birika eeh, nilidhani mbwangu kumbe*

*Ni bwa shirika*

Ubeti huo umebeba ujumbe kwa mume na mkemwenza wa mwimbaji. Mwimbaji anamlinganisha mume wake na mkorosho pia na kurudia maneno aliyoyasema katika ubeti wa tatu. Mama anamkemea mkemwenza kwa kusema ni hasidi aliyeupiga mkorosho wake moto. Mama anatumia mimea ya mkorosho na mbatata kuonyesha vile ambavyo aliishi na mume wake akimtunza vile ambavyo mimea hii hutunzwa lakini pakatokea mtu akaikanyaga. Kwa mujibu wa wasailiwa, mbatata ni malenge, lakini alitokea hasidi, mtu mwenye wivu akaulizata kwa maana ya kuwa akaukanyaga maksudi ili usiendelee kukua. Anasema pia kwamba alikuwa na mkorosho wake kisha akatokea hasidi akaupiga moto. Mwimbaji anaeleza vile alivyokuwa akihangaika kumwandalia mume wake chai akifikiri ndiye alikuwa mke wake wa pekee kumbe alikuwa mume wa shirika.

Ujumbe katika ubeti ufuatao wa sita unalenga mtoto. Mama anambembeleza mtoto huku akimhimiza kulia ili ambembeleze na kumpa ng'ombe aliye na pembe kubwa. Katika ubeti huu, mama anamwahidi mwanawe ng'ombe wa pembe kubwa. Hali hii inajitokeza pia katika baadhi ya bembelezi ulimwenguni kama vile za Kihispania, Kituruki na Kialbania ambamo watoto walipewa ahadi nyingi iwapo wangetulia au kunyamaza kama wanavyosema Esteve na wenzake (2014), Doja (2015), Mingazova na Sulteev (2014). Kwa hivyo ahadi za uongo kwa mtoto katika bembelezi ulikuwa mkakati wa kumshawishi mtoto kutulia na ni jambo linalodhihirika katika bembelezi ulimwenguni.

*Nchocho haaao, nchocho haaao x2*

*Nchocho lia, lia nikupembeoo*

*Nikupembe, nikupe na ng'ombe*

*Nkuru wa pembe*

Katika mshororo wa tatu wa ubeti wa mwisho ufuatao, ujumbe unamlenga mtoto. Mwimbaji anamweleza mtoto kuwa asifikiri kwamba amenyamaza kwa kuwa haelewi kinachoendelea, la hasha! Anafahamu mengi yanayoendelea na hata alipata kuyasikia yote yaliyofanyika Amu.

*Nchocho haaao nchocho haaao x2*

*Nchocho lia, lia nikupembe*

*Sinione kunyamaa, si nchache wa fahamu*

*Sikuwata kusikia mambo yalojiri Amu*

*Yalovava kisimani na mtungini si tamu*

Ujumbe katika mshororo wa mwisho ni wa kimafumbo. Mama anasema mkemwenza wake hakuwa mwanamke mtulivu. Alikuwa kama maji ya kisimani yaliyo na chumvi, yakiwekwa mtungini, ladha ile ya chumvi haiishi. Hivyo basi tabia za yule mkemwenza za kubadilisha wanaume zisingekoma hata katika ndoa, asingetulia, angeendelea na hizo tabia.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

Kimsingi, walengwa wa bembelezi za tamaduni mbalimbali ulimwenguni ni watoto kwa sababu nyimbo zenyewe ni za watoto pia. Inadhihirika wazi kutokana na matokeo ya utafiti kwamba walengwa wa ujumbe katika bembelezi za Watikuu ni wanajamii tofauti. Bembelezi za jamii hii zinaonyesha kuwa wanawake huzitumia kulalamika, kueleza au kutoa hisia zao kuhusu wanajamii waliowakosea; baadhi ya walengwa huwa majirani, baba, mama, mavyaa, wifi, mtoto, wanawari na wengineo.

Waandishi wanapendekeza bembelezi za Watikuu zitafitiwe zaidi kwa mtazamo wa kimawasiliano kwa sababu matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba wanawake katika jamii hii huzitumia kama chombo cha mawasiliano. Ni bayana kuwa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.817

wanatumia bembelezi kama jukwaa la mawasiliano wanapotoa hisia zao kuhusu watu waliowakosea yanafanya nyimbo hizi ziwe kama jukwaa linalosaidia kuleta suluhu ya amani miongoni mwa wanawake wanapokosana au kati ya wake na waume zao bila kukabiliana ana kwa ana.

**MAREJELEO**


Abdalla, A. (2012). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press. (uk vi)

Doja, A. (2015). Socializing Enchantment: A Socio-Anthropological Approach to Infant Directed Singing, Music Education and Cultural Socialization. In *International Review of the Aesthetics and Sociology of Music, JSTOR,45(1),115- 147.*

Esteve-Faubel, J. M., Esteve-Faubel, R. P., Cavia-Naya, V., & Benlloch, M. T. O. (2014). Women's Songs: The Lullaby in the Spanish Autonomous Region of Valencia. Western Folklore, 69-116.

Gunes, H., & Gunes, N. (2012). The Effects of Lullabies on Children. In *International Journal of Business and Social Science. 3*(7), 316 – 321.

Hassan, S. (2010). Female traditional singers in Iraq: A survey. *International Journal of Contemporary Iraqi Studies*, *4*(1-2), 25-39.

Akyol, P. K. (2014). Today’s Lullabies and Lullaby Tradition Shaped by the Effect of Cultural change and Technology. *Katika Bilig: Social Sciences Journal*, *1*(69), 127- 142.

Kaya, S. Ö. & Özkut, B. (2016). The Influence of Developing Technology and Mother’s Songs: Lullabies. *In International Journal of Human Sciences,* 13(1), 778-786.

Loewy, J., Stewart, K., Dassler, A. M., Telsey, A., & Homel, P. (2013). The Effects of Music Therapy on Vital Signs, Feeding, and Sleep in Premature Infants. Pediatrics, 131(5), 902-918.

Mackinlay, E. & Baker, F. (2005). Nurturing Herself, Nurturing Her Baby: Creating Positive Experiences for First-time Mothers through Lullaby Singing," *Women and Music*, 9, Pp 69-89.

Mingazova, L., & Sulteev, R. (2014). Tatar and English Children's Folklore: Education in Folk Traditions. *In Western States Folklore Society*, 73(4). 410- 431.

Saville-Troike, M. (2003). Ethnography of Communication: An Introduction. 3rdEdition. London: Blackwell Publishing.

Senkoro, F. E. M. K. (2005). Understanding Gender through Genre: Oral literature as a Vehicle for Gender Studies in East Africa. *Gender, Literature and Religion in Africa*, *4*(1), 1-10.

Trehub, S. E., & Prince, R. L. (2002). Mothers as Musical Mentors. *Journal of Zero to Three*, *23*(1), 19-22.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.